

Aina mbalimbali za Vitendo vya Unyanyasaji wa Kijinsia

- Unyanyasaji wa kijinsia ni ukiukaji wa haki za binadamu (rejea Azimio lenye ujumbe : "Ukatili dhidi ya Wanawake" lililopitishwa na mkutano wa 60 wa Tume ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa mwaka 2004).
- Kimataifa, Unyanyasaji wa Kijinsia unatafsiriwa kama "kitendo chochote cha kumkaribia mtu kwa nia ya kumshawishi kufanya tendo la kujamiiana ambacho hakishawishiki, hakikusudiki na ambayo hakikubaliki". Urubunifu huu unatokana na matendo yanayoashiria hisia mbaya, ukaribu na migusano isiyo sahihi, muonekano unaoshawishi na shinikizo la mahusiano ya kimapenzi au vidokezo vinavyoashiria vitendo vya kujamiiana.
- Vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia vinatokea katika maeneo yote kwenye jamii na matendo haya yanatokana na kutoheshimu hadhi ya utu na badala yake watu wamefananishwa na vitu visivyo hai. Vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia vinatokea katika maisha ya kila siku kwenye mikusanyiko ya watu, nyumba za wageni, familia, maeneo ya warsha na kwenye jamii za kidini pamoja na mashirika. Wengi wa waathirika wa vitendo hivi vya unyanyasaji wa kijinsia ni wanawake.



United Evangelical Mission
Communion of churches
in three Continents

United Evangelical Mission (UEM)
Communion of Churches in three Continents
Rudolfstrasse 137
42285 Wuppertal
Germany

Fon +49 (0) 202 / 890 04-0
Fax +49 (0) 202 / 890 04-79
info@vemission.org
www.vemission.org



Hitimisho

Waraka huu unakusudia kuwahusisha wanachama wote wa UEM juu ya tatizo la Unyanyasaji wa kijinsia na kuwashawishi kushughulikia jambo hili. Hivyo basi waraka huu utasambazwa kwenye makanisa na utatolewa kwa lugha za Kingereza, Kifaransa, Kijerumani, Kiindonesia-Bahasa na Kiswahili. Waraka huu umeandikwa na Tume ya Jinsia na umepitishwa na Mkutano Mkuu wa UEM uliofanyika Borkum/Ujerumani mwaka 2008.

Imechapifwa na
United Evangelical Mission (UEM)
Picha: Fotolia - Imeandaliwa na: MediaCompany GmbH - Imesahihishwa: Juli 2010



»Unyanyasaji wa Kijinsia ni ukiukwaji wa Haki za Binadamu«

Kanuni za Maadili Mema ya UEM

Biblia inathibitisha kwamba wanawake na wanaume wa tamaduni zote, mataifa yote na dini zote wameumbwa sawa kwa mfano wa Mungu. Kila kiumbe hai kimepata hadhi yake kama zawadi ya Mungu. Huu ni msingi wa heshima kwenye mahusiano kati ya mwanaume na mwanamke.

SIMU YA MOJA KWA MOJA:

Dibaji

Biblia inathibitisha kwamba wanawake na wanaume wa tamaduni zote, mataifa yote na dini zoto wameumbwa sawa kwa mfano wa Mungu. Kila kiumbe hai kimepata hadhi yake kama zawadi ya Mungu. Huu ni msingi wa hesima kwenye mahusiano kati ya mwanaume na mwanamke.

Hii ni moja ya misingi ya imani za kithiolojia ambayo inatumika na wanachama 35 toka Afrika, Asia na Ujerumani ambao kwa pamoja wanajenga Muungano wa Misioni ya Uinjilisti yaani UEM.

Jinsi ya kuepuka Vitendo vya Unyanyasaji wa Kijinsia

- Heshimu jinsia nyingine na usitumie vibaya mahusiano binafsi, ya kikazi au aina yoyote nyingine ya mahusiano.
- Tambua ya kwamba mtu mwenye mamlaka ana wajibu maalum.
- Fahamu tofauti na desturi za kitamaduni
- Usivuke mipaka ambayo imewekwa na wengine. Kama mtu fulani anasema “HAPANA” ni lazima uheshimu.
- Kataa vitendo vinavyoashiria hisia au kugusana na mtu wa jinsia tofauti na yako ambavyo sio sahihi. Onyesha kwamba tabia kama hiyo haikubaliki.
- Wajulishe watu kama vitendo hivi vinatokea katika jamii.
- Eleza tatizo lako kwa mtu unajemuamini.
- Usishutumu watu kiunafiki kwa vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia kwa faida yako
- Mbele ya waraka huu unaweza kupata namba ya simu ya moja kwa moja katika eneo lako, ambayo ni lazima uitumie pindi tendo la unyanyasaji wa kijinsia linapotokea.
- Tumia mara moja namba hiyo ya simu ya moja kwa moja iwapo mtu fulani amekushutumu kwa tabia za kubugudhi kwa kukusingizia.



Hatua gani za kuchukuwa?

- Kufanyike uteuzi wa watu wawili ambao ni wawajibikaji (mwanamke na mwanaume) watakaosimamia “Kamati ya Nidhamu”. Uteuzi huu ni lazima uzingatiwe mwanzoni mwa vikao vyote, kwenye kongamano na warsha zote.
- Kama kuna mashitaka yaliyoletwa ni lazima yachunguzwe na yashughulukiwe kwa uangalifu na umakini. Swala hili lishughulikiwe kwa siri na kamati ya nidhamu kwa kuhusisha pande zote mbili yaani mlalamikiwa na mlalamikaji.
- Kuhusu muathirika mipango iwekwe ya kumpatia ushauri na huduma ya kichungaji.
- Katika aina yoyote ya unyanyasaji wa kijinsia ni vyema muathirika akasaidiwa katika hatua za kisheria.
- Mlalamikiwa ni lazima aondolewe kwenye kikao na asiruhusiwe kubaki kwenye maeneo ambako ana nafasi ya kurudia makosa haya.
- Mlalamikiwa lazima pia apate ushauri na huduma za kichungaji.